



JAMUHURI YA MUUNGANO
WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA,
MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO

BARAZA LA FAMASI

UHUISHAJI WA TAARIFA ZA WANATAALUMA WALIOPO KWENYE REJESTA KWA
MWAKA 2022 NA UPATIKANAJI WA LESENI ZA UTENDAJI KAZI KWA MFUMO WA
KIELEKTRONIKI

UTANGULIZI

1. **DHUMUNI:** Kutekeleza takwa la Kifungu Na. 22, 26 na 30 vya Sheria ya famasi ya mwaka 2011 (*The Pharmacy Act 2011*) Sura 311.
2. **WAHUSIKA:** Wafamasia, Fundi Dawa Sanifu na Fundi Dawa Wasaidizi.
3. **MFUMO WA UHUISHAJI:** Mfumo wa kielektroniki utamtaka mwanataaluma kuwasilisha taarifa zake za sasa kwa Msajili kwa mujibu wa Sheria na kudurufu (printing) leseni yake ya utendaji kazi ya kielektroniki.

LENGO LA UTARATIBU

1. **BARAZA:** Kurahisisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa haraka.
2. **WANATALUUMA:** Kupunguza gharama na upotevu wa muda kwa ajili ya ufuwatiliaji wa taratibu, uwasilishaji wa taarifa na upatikanaji wa leseni.

UTARATIBU WA KUHUISHA TAARIFA ZA MWANATAALUMA KWENYE
REJESTA

- a) **FOMU:** Ingia katika tovuti ya baraza www.pc.go.tz kisha bonyeza huduma za kimtandao (*Online Services menu*) kisha bonyeza *Retention Application*; (*Sign up*)
<http://196.45.42.57:8081/pcmis.data/view/modules/registration/pharmacist-signup.php>
Sign in: <http://196.45.42.57:8081/pcmis.data/>
- b) **ADA:** Lipa ada ya kushikilia jina kwa mujibu wa Kanuni za Usajili wa Wanataaluma ya mwaka 2005 na Kanuni za Ada na Tozo ya mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2012 kama ifuatavyo:-

Mfamasia.....TZS 165,000/-
 Fundi dawa sanifuTZS 66,000/-
 Fundi dawa msaidizi..... TZS 44,000/-

- c) **MUDA WA MALIPO:** Mwisho wa kulipia ada ni tarehe 31/12/2021, baada ya hapo utalazimika kulipa pamoja na faini ya asilimia ishirini na tano (25%) ya kiwango alichotakiwa kulipia.

MAMBO YA KUZINGATIWA WAKATI WA KUHUISHA TAARIFA ZAKO KWENYE REJESTA

- a) **JINA:** ni kwa mujibu wa cheti cha usajili (Registration, Enrollment, or Enlisting certificate);
 b) **NAMBA YA USAJILI** (Registration, Enrollment or Enlisting Number): imetoholewa na kutoa Personal Identification Number (PIN) kwa mifano ifuatayo:-

S/N	KADA	NAMBA YA USAJILI	KEY CODE	PIN (PERSONAL IDENTIFICATION NUMBER)
1.	Mfamasia	754	01	00000 mfano 0100754
2.	Fundi Dawa Sanifu	1010	04	00000 mfano 0401010
3.	Fundi Dawa Msaidizi	24	05	00000 mfano 0500024

Hata hivyo kwa wale ambao wana leseni tayari PIN zimeanishwa kwenye vitambulisho hivyo.

- c) **PICHA:** wasilisha (*upload*) nakala laini ya picha ya uso (*passport size*) yenye *Blue Background* zingatia vipimo *width 350px height 350px*.
- d) **MAFUNZO ENDELEVU** (*additional qualification*): wasilisha nakala laini ya vyeti vya mafunzo endelevu aidha kozi za muda mrefu na muda mfupi;
- e) **LESENI YA UTENDAJI KAZI:**
- I. Baraza limeandaa utaratibu mpya wa uandaaji na uchapishaji wa leseni za utendaji kazi, ambazo kwasasa zitatolewa kwenye mfumo wa Baraza kupitia akaunti ya mwanataaluma aliyoitumia kufanya maombi ya kuhuisha taarifa kwenye rejesta kwa njia ya kielektroniki.

II. Baada ya mwanataaluma kukamilisha maombi ya kuhuisha taarifa kwenye rejista, ataweza kudurufu (printing) leseni yake ya utendaji kazi katika karatasi ya kawaida.

NOTE: Mwanataaluma ambaye alishahuisa taarifa zake kwenye rejista kwa mwaka 2021 sasa anaweza kudurufu (printing) leseni yake ya utendaji kazi ambayo itakwisha muda wake tarehe 31/12/2021 hadi hapo atakapofanya maombi ya kuhuisha taarifa kwa mwaka 2022.

f) **MALIPO:**

- (i) *Control Number* itapatikana kwenye mfumo (*automatically*) wakati wa kuwasilishwa maombi sehemu ya *Bill Creation* na kutumwa kwenye namba yako ya simu.
- (ii) *Control Number* hii itakuwa na uhai ambao utakoma matumizi tarehe 31/12/2021.
- (iii) Tembelea akaunti yako sehemu ya *Bill Creation* kuweza kupata namba mpya ya malipo baada ya tarehe 31/12/2021 ambayo itaambatana na faini ya 25%:

g) **USER MANUAL:** Kabla ya kuanza kujaza taarifa zako kwenye *Pharmacy Council Online Retention Application System (PCORAS)* hakikisha unasoma *User Manual*
<https://www.pc.go.tz/files/PharmaceuticalPresonnelRetentionUserManual.pdf>

Imetolewa na:

Msajili, Baraza la Famasi

S.L.P. 1277, Dodoma Simu: 0736 222 515

Toll Free Number: 0800110015

Barua pepe: info@pc.go.tz /registration@pc.go.tz